

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mtaa wa Mahakama,

S. L. P. 1419,

53103 MBEYA.

Simu: (025) 252503566

Nukushi: (025) 252502958

Barua pepe: [rbcmbeya@pcb.go.tz](mailto:rbcmbeya@pcb.go.tz)

Wavuti: <http://www.pcb.go.tz>

## TAARIFA KWA UMMA

---

**MBEYA – AUGOSTI 18, 2020**

### **TAKUKURU MBEYA YAZIDI KUOKOA FEDHA TOKA KWA WADAIWA SUGU**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Rungwe Mkoani Mbeya imefanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi milioni themanini na sita mia moja hamsini na tisa elfu na mia saba hamsini (**86,159,750.00**) zilizokuwa zimefanyiwa ubadhilifu katika vyama vitano vya ushirika (AMCOS NA SACCOS) Wilayani hapo.

Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Rungwe - Mohamed Shariff kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Rungwe Mhe. Chalya Julius wamekabidhi fedha hizo Agosti 18, 2020 kwa viongozi baada ya kuokolewa toka kwa wadaiwa sugu kwa mchanganuo ufuatao:-

1. KYIMO SACCOS kiasi cha shilingi milioni ishirini na tatu mia mbili themanini na nne elfu na mia sita hamsini (23,284,650.00)
2. KIWIRA SACCOS kiasi cha shilingi milioni hamsini na moja mia saba sabini na mbili elfu na mia tisa (51,772,900.00)
3. IKUTI SACCOS kiasi cha shilingi milioni saba ishirini na tano elfu na mia saba (7,025,700.00)
4. AMANI MALANGALI SACCOS kiasi cha shilingi milioni moja laki moja kumi na mbili elfu na mia tano (1,112,500.00)
5. ISEMPU AMCOS kiasi cha shilingi milioni mbili laki tisa sitini na nne elfu (2,964,000.00)

## **WITO KWA WANANCHI**

Tunawapongeza wananchi wa Wilaya ya Rungwe na mkoa wa Mbeya kwa ujumla kwa kuendelea kushirikiana na Taasisi yetu katika mapambano dhidi ya rushwa. Tunawaasa wale wote ambao wanadaiwa madeni kwenye AMCOS na SACCOS zote kuhakikisha kwamba wanarejesha fedha wanazodaiwa kabla TAKUKURU haijachukua hatua dhidi yao.

**IMETOLEWA NA:**

**JULIETH MATECHI  
MKUU WA TAKUKURU MKOA WA MBEYA**

---